# Mahitaji ya Chanjo katika California ya Shule ya Chekechea hadi Gredi ya 12

Shule za California zinahitajika kuangalia rekodi za chanjo kabla ya kumsajili mtoto shuleni. Mahitaji yanayofuata ya chanjo lazima yatimizwe kabla ya mwanafunzi kuweza kujisajili au kuhudhuria shule. Mahitaji haya lazima pia yatimizwe mtoto akihama kwenda shule nyingine mpya, anapoanza Chekechea, Shule ya Chekechea ya Mpito, Chekechea na/au gredi ya 7.

**UNACHOHITAJI:**

Wakati wa usajili, utahitaji rekodi ya chanjo inayoonyesha kuwa mtoto wako amepokea chanjo zote zinazohitajika. Fomu zinazofuata zinakubalika katika uthibitisho:

1. Rekodi ya Chanjo ya California
2. Fomu nyingine ya rekodi ya chanjo kutoka kwa daktari wako iliyo na tarehe ambayo mtoto wako alipokea kila chanjo

Katika kiwango cha chini zaidi, rekodi hiyo lazima ionyeshe mwezi na mwaka wa kila chanjo. Huenda ukahitaji kupiga simu kwa daktari au kliniki yako ili kupata hati hii.

- Vipimo vya maabara havitimizi mahitaji haya na kwa hivyo haviwezi kutumika kama ithibati ya chanjo.

**CHANJO ZINAZOHITAJIKA KULINGANA NA SHERIA YA JIMBO:**

| CHANJO | DOZI | VIDOKEZO |
|---|---|---|
| Polio | dozi 4 | • Dozi 3 ni sawa iwapo alipewa mwaka wa au baada ya kufikisha miaka 4<br>• dozi 3 ni sawa iwapo mwanafunzi ana umri usiozidi miaka 5 |
| DTaP | dozi 5 | • Tdap au Td iwapo ana umri wa miaka 7 au zaidi<br>• Dozi 4 ni sawa iwapo alipewa mwaka wa AU baada ya kufikisha miaka 4 au mwanafunzi ana umri usiozidi miaka 5<br>• Dozi 3 ni sawa iwapo ya mwisho alipewa mwaka wa au baada ya kufikisha miaka 7.<br>• Angalau dozi moja lazima iwe ya Tdap au DTaP/DTP iliyopeanwa mwaka wa au baada ya miaka 7 kwa wanafunzi wote wa gredi ya 7 hadi 12 |
| Homa ya Manjano B | dozi 3 | • Haihitajiki wakati wa kuingia gredi ya 7 |
| MMR | dozi 2 | • Dozi zote mbili zinapeanwa wakati wa kufikisha au baada ya kufikisha mwaka 1<br>• Dozi 1 ni sawa iwapo mwanafunzi ana umri usiozidi miaka 5 |
| Varicella (Tetekuwanga) | dozi 2 | • Historia ya ugonjwa **HAITOSHI** kuondoa mahitaji ya chanjo hii.<br>• Kinzano cha Kudumu cha Matibabu cha Chanjo kinahitajika (CAIR-ME)<br>• Dozi 1 ni sawa iwapo mwanafunzi ana umri usiozidi miaka 5 |
| Tdap (Gredi ya 7/8) | dozi 1 | • Au DTP/DTaP iliyopeanwa mwaka wa au baada ya miaka 7 |
| Hib (Kwa Utunzaji wa Watoto/Kabla ya Chekechea pekee) | dozi 1 | • Dozi moja ipeanwa wakati wa kufikisha au baada ya kufikisha mwaka 1<br>• Dozi mbili ni sawa iwapo umri hauzidi miezi 14 |

| DOZI | USIJUMUISHE IWAPO HAIJAPEANWA KUFIKIA | |
|---|---|---|
| Polio #2 | Wiki 8 baada ya dozi ya 1 | |
| Polio #3 | Miezi 12 baada ya dozi ya 2 | |
| Polio #4[1] | Miezi 12 baada ya dozi ya 3 | |
| DTaP #2 | Wiki 8 baada ya dozi ya 1 | |
| DTaP #3[2] | Wiki 8 baada ya dozi ya 2 | |
| DTaP #4[3] | Miezi 12 baada ya dozi ya 3 | |
| DTaP #5 | Miezi 12 baada ya dozi ya 4 | |
| Hep B #2 | Wiki 8 baada ya dozi ya 1 | |
| Hep B #3 | Miezi 12 baada ya dozi ya 2 na angalau miezi 4 baada ya dozi ya 1 | |
| MMR #2 | Miezi 4 baada ya dozi ya 1 | |
| Varicella #2 | Miezi 4 baada ya dozi ya 1<br>Chini ya miaka 13 | Wiki 8 baada ya dozi ya 1<br>Zaidi ya miaka 13 |

Je, mtoto wako amepokea chanjo zote zinazohitajika? Iwapo hajapokea, tafadhali kuwa na miadi na daktari wako au kliniki ya chanjo katika Idara ya Afya ya Umma katika Kaunti ya San Diego. Beba rekodi zako unapoenda kwenye miadi hii. Iwapo mtoto wako hajapokea chanjo zote zinazohitajika shule itakapoanza, mtoto wako, kisheria **hatakubaliwa** kwenye shule.

**Ratiba ya Usajili katika Gredi za EAK/TK/K-12**

Kabla ya usajili mtoto ni lazima apate dozi ya kwanza ya kila chanjo inayohitajika na dozi zozote zitakazofuata kwa sababu kipindi cha muda kinachokubaliwa kabla ya kutojumuishwa kimeisha.

**Imani ya Kibinafsi ya Kutojumuishwa (PBE)**

PBE **HAZIKUBALIWI** tena

**Kinzani za Kimatibabu**

Kinzani ya kimatibabu (ya muda au kudumu) iliyotolewa kupitia CAIR-ME, iliyokamilishwa na kuchapishwa na daktari wa mtoto wako (MD au DO aliye na leseni California), iwapo yoyote kati ya channjo hizi hazikupeanwa kwa mtoto wako kutokana na sababu za kimatibabu.

- Kinzani za muda za matibabu hazitazidi miezi kumi na miliwi ya kalenda kuanzia tarehe ambayo daktari aliye na leseni aliandika taarifa